# JARIDA LA UWEZESHAJI

*Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)*

*JANUARI,* 2018

**TOLEO LA TANO**

## MKAKATI WA KUENDELEZA UJASIRIAMALI NCHINI WAZINDULIWA



***NEEC yaingia makubaliano na PPRA kuwainua wazabuni wa ndani (uk. 17)***



***Baraza ladhamini Mkopo wa milioni 360 kwa Mbunifu wa viwanda (uk. 7 )***

# YALIYOMO

**HABARI** **UKURASA**

1. Neno kutoka kwa Katibu Mtendaji……………………………..………....3

2. VICOBA kanda ya ziwa vyapata mkopo wa bilioni 2.8 ………………...5

3. Baraza ladhamini mkopo wa milioni 360 kwa mbunifu wa viwanda……7

4. Siku ya VICOBA yazinduliwa rasmi nchini………………………...........10

5. Baraza latoa mafunzo ya uanzishwaji wa madawati ………..……....13

6. Profesa Kamuzora awahasa Watanzania kupiga vita umasikini ………..16

7. NEEC yaingia makubaliano na PPRA kuwainua wazabuni wa ndani .....17

8. Mkakati wa kuendeleza ujasiriamali wazinduliwa ……………………..19

9. Habari katika picha……………………..……………………………..21

# Neno kutoka kwa Katibu Mtendaji

Ndugu msomaji wa Jarida la Uwezeshaji,Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) linakutakia heri na Baraka katika mwaka mpya wa 2018.




Karibu kwa mara nyingine katika toleo letu la tano linalohusu shughuli za Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na mafanikio yake katika mwaka wa 2017 pamoja na dira mpya ya mwaka 2018 katika kuhakikisha sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 iliyo chini ya kifungu namba 16 inatekelezwa.

Baraza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa masuala ya Uwezeshaji limezidi kutanua wigo wa utekelezaji wa sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi baada ya kufanikisha uzinduzi wa Mkakati wa Taifa wa kuendeleza Ujasiriamali nchini.

Tunafurahi kufanikisha uzinduzi huo ambao utakuwa chachu ya kusukuma mbele dira ya Serikali ya awamu ya tano katika kuifanya Tanzania ya viwanda na kufikia uchumi wa kati.

Baraza pia limefanikisha kusaini rasimu ya makubaliano na Taasisi ya manunuzi ya Umma (PPRA) ili kulinda maslahi ya wazabuni wadogo kunufaika na tenda zinazotangazwa katika ofisi za Serikali.

Baraza limefikia makubaliano hayo ili kuleta usawa kwa wazabuni wazawa kunufaika na zabuni zinazotolewa na ofisi za Umma.

*inaendelea uk.4*

Katika kutekeleza sera ya Uwezeshaji Wananchi kwa vitendo, Baraza limeendelea kutoa dhamana ya mikopo kwa vikundi vya uzalishaji mali kupitia mfuko wa Mwananchi.

Baraza linaratibu kazi hii kwa ushirikiano wa karibu na taasisi za fedha za UTT Mircofinance na Benki ya Posta hapa nchini.

Baraza liliendelea na ziara zake katika mikoa ya kanda ya ziwa inayojumuisha mikoa ya Kagera,Geita, Mwanza,Simiyu na Mara na kuvifikia vikundi 228 vya uzalishaji mali ambavyo vinajiendesha kwa mfumo wa VICOBA na SACCOS.

Katika ziara hiyo, Baraza lilitoa dhamana ya jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.8 kupitia taasisi za fedha za UTT Microfinance na Benki ya Posta.

Kwenye sekta ya viwanda na kilimo, Baraza limefanikiwa kumuwezesha mbunifu wa viwanda Bwana George Buchafye ambaye ni Mkuugenzi wa Kampuni ya Star Natural Product dhamana ya mkopo wa Shilingi milioni 50 kupitia taasisi ya fedha ya UTT Microfinance.

Fedha hiyo inatarajia kuongezeka mpaka kufikia shilingi milioni 360 kulingana na utekelezaji wa mradi.

Katika mkopo huo, kampuni ya Star Natural Product itawajibika kutengeneza mashine za kuchakata mazao ya alizeti na michikichi na kuzisambaza kwa vikundi vya wakulima ili kuongeza uzalishaji wa mazao hayo ya biashara na kupandisha thamani ya bidhaa za Tanzania

Mwaka huu wa 2018 Baraza litaendelea kuratibu Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kufikia namba kubwa ya Watanzania ili kila mzawa anufaike na fursa za uwezeshaji zilizopo.

Baraza linasisitiza matumizi bora ya Mkakati wa Taifa wa kuendeleza Ujasiriamali nchini ambao ulizinduliwa kwa ushirikiano mzuri na UNCTAD.

**Bi Bengi Issa**
**Katibu Mtendaji**

# VICOBA kanda ya ziwa vyapata mkopo wa Bilioni 2.8




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na watu wenye ulemavu,Mheshimiwa Jenista Mhagama akikabidhi hundi kwa taasisi ya VISUDENT iliyopo Kanda ya Ziwa.*

Vikundi 271 vya VICOBA kutoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa vimenufaika na dhamana ya mikopo kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia taasisi za fedha za UTT Microfinance PLC na Bank ya Posta (TPB).

Vikundi hivyo vinavyotoka katika Wilaya za Mikoa ya Kagera,Geita, Mwanza, Simiyu na Mara vimepata dhamana ya mikopo yenye masharti nafuu ya jumla ya shilingi Bilioni 2.8.

Akizungumza wakati wa utoaji wa mikopo hiyo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na watu wenye ulemavu,Mheshimiwa Jenista Mhagama amesema kuwa dhamana ya mikopo hiyo ni sehemu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambapo imetolewa ili kuwafanya wanavikoba waweze kuendeleza miradi mbalimbali ya ujasiriamali.

"Huu ni uwezeshaji mkubwa na tunataka mikopo hii itumike kuendeleza miradi ya ujasiriamali na kuzalisha faida ili kuondokana na hali duni za kimaisha"alisema Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Mheshimiwa Jenista Mhagama pia alizitaka taasisi zingine za fedha kufika katika halmashauri na kutoa huduma za mikopo kwa wananchi ili waweze kuzitumia katika shughuli za ujasiriamali na kwa kufanya hivyo Taasisi hizo zitaweza kujiongezea idadi ya wateja huku pia wakisaidia jitihada za Serikali kukwamua wananchi kiuchumi.

Katika mikopo hiyo, TPB imetoa bilioni 2.7 kwa vikundi 228 na UTT Microfinance imetoa Tsh 100, 300, 00 kwa vikundi viwili vyenye wanachama 30.

Katibu Mtendaji wa Baraza, Bi Beng'i Issa alisema kuwa mikopo hiyo imedhaminiwa kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na imeletwa kwa masharti nafuu kwa vikundi vinavyojiendesha kwa mfumo wa SACCOSS na VICOBA.

"Vikundi hivi ni matunda ya taasisi Mwamvuli zilizokubali kushirikiana na Serikali kuvianzisha na kufundisha elimu ya VICOBA, Serikali itaendelea kushirikiana na Taasisi hizi katika kazi ya kuwawezesha Wananchi"alisema Katibu Mtendaji.



*Wanachama wa Vikoba wakifuatilia maelekezo kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na watu wenye ulemavu,Mheshimiwa Jenista Mhagama wakati wa zoezi la utoaji wa mikopo.*

# Baraza ladhamini mkopo wa Milioni 360 kwa Mbunifu wa Viwanda




*Mkurugenzi wa Kampuni ya Star Natural Product, Bwana George Buchafye akikabidhiwa hundi na Mkurugenzi wa UTT Microfinance Bwana James Washima baada ya kupata dhamana ya mkopo kutoka Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kushoto ni Katibu Mtendaji Bi Beng'i Issa.*

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limedhamini mkopo wa Tshs 360 Milioni kupitia Taasisi ya fedha ya UTT Microfinance PLC kwa Kampuni ya Star Natural Product Limited ambayo inamilikiwa na mjasiriamali wa Kitanzania Bwana George Buchafye.

Dhamana ya mkopo iliyotolewa na Baraza imelenga kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kutengeneza sabuni, kuchakata zao la alizeti na mchikichi ili kuzalishia mafuta ya kupikia toka kwenye makundi mbalimbali ya wazalishaji mali.

Mkopo huo umetolewa kwa awamu kulingana na utekelezaji wa wazo la mradi ambapo kwa awamu ya kwanza mjasiriamali George Buchafye alikabidhiwa hundi ya Tsh Milioni 50 kwa ajili ya kufanikisha wazo lake la uanzishaji wa viwanda.

Mbunifu huyo wa viwanda ambae anafanyakazi chini ya SIDO atatakiwa kuunda vikundi vya uzalishaji mali na kuvipa elimu ya kutumia mashine alizobuni ili wanavikundi waweze kujikwamua kiuchumi na kupiga hatua kimaisha.

Baraza linatarajia mradi huo utachochea kasi ya ukuaji wa viwanda na uzalishaji wa malighafi za kilimo cha alizeti na mchikichi huku vipato vya wakulima vikiongezeka kwa kiwango kikubwa.

Wakati wa makabidhiano ya hundi, Katibu Mtendaji wa Baraza Bi Beng'i Issa aliwataka Watanzania kuwa wabunifu katika uanzishaji wa viwanda ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuongeza pato la Taifa.

Katibu Mtendaji alipongeza jitihada za kampuni ya Star Natural Product kwa kudhamiria kupunguza tatizo la ajira na kubuni wazo la uanzishaji wa viwanda ambalo linaendana na maono ya Serikali ya awamu ya tano.

Bi Beng'i alisisitiza juu ya uaminifu kwa Watanzania pindi wanapopewa dhamana ya mikopo warejeshe kwa wakati muafaka ili wengine waweze kunufaika na fursa ya dhamana hizo za mikopo.

Nae Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Fedha ya UTT Microfinance PLC, Bwana James Washima amehaidi kuendelea kushirikiana na Baraza la Uwezeshaji katika kutoa mikopo kwa vikundi vya uzalishaji mali ili kuendeleza shughuli za kiuchumi na kutanua wigo wa ajira kwa vijana wa Tanzania.

Mkurugenzi wa Star Natural Product, Bw George Buchafye ameshukuru jitihada zilizofanywa na Baraza katika kutoa dhamana za mikopo kwa wananchi huku akihaidi kutekeleza lengo la maombi ya mkopo huo kwa kuwekeza kwenye kutoa mafunzo kwa vikundi mbalimbali vya wajasiriamali nchini wenye lengo la kujikita katika ubunifu na uundaji wa mashine za kuchakata mazao ya mafuta na utengenezaji wa sabuni.

Bwana Buchafye amesema kwamba atahakikisha mashine zake anazisambaza mikoani kwa vikundi vya wakulima ili kurahisisha ukamuaji wa mafuta ya mazao sambamba na kuwapa elimu juu ya matumizi ya mashine hizo.

Zoezi la makabidhiano ya hundi lilifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Baraza la Uwezeshaji Jijini Dar es salaam likishuhudiwa na wanahabari, watendaji wa Baraza na wawakilishi wa UTT Microfinance PLC.




*Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Bibi Bengi'Issa akizungumza jambo katika mkutano wa makabidhiano ya hundi na Mbunifu wa viwanda bwana George Buchafye*




# Siku ya VICOBA yazinduliwa rasmi nchini

KATIKA kufanikisha jitihada za Serikali ya awamu ya tano ili kukuza uchumi wa Taifa, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kwa kushirikiana na taasisi mwamvuli za VICOBA FETA,IR VICOBA na TIMAP wamefanikiwa kuzindua siku ya VICOBA Tanzania ambayo itakuwa ikifanyika kila Octoba 17 ambayo ni siku ya Kimataifa ya kutokomeza umasikini Duniani.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Baraza kutambua mchango mkubwa wa VICOBA hapa nchini katika kutoa huduma za kifedha kwa wananchi wa vijijini na mijini ili kutokomeza lindi la umasikini kwa kuwawezesha kiuchumi.

Mpaka hivi sasa kuna wanachama takribani milioni 2.2 kutoka kwenye vikundi 100,000 ambavyo vinachangia moja kwa moja katika pato la Taifa vikiwa na amana ya Tshs 1.3 trilioni huku wanachama hao asilimia themanini wakiwa ni wanawake na ishirini ni wanaume.

Wajasiriamali kutoka kwenye vikundi vya VICOBA walipata fursa ya kunadi bidhaa zao ili kutanua wigo wa masoko katika viwanja vya mnazi mmoja ambapo shughuli hiyo ilizinduliwa na mgeni rasmi Mheshimiwa Charles Mwijage ambaye ni Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya siku ya VICOBA kilifanyika katika ukumbi wa Mlimani City ambapo mgeni rasmi alikuwa ni waziri wa Fedha na Mipango, mheshimiwa Philip Mipango ambaye pamoja na kutoa pongezi lakini pia alihaidi kufanyia kazi changamoto zinazowakabili wana VICOBA hapa nchini.

Katika ukumbi wa Mlimani City kulikuwa na mada mbalimbali zilizoibuliwa na wataalamu wa masuala ya uchumi wakiwemo Bwana George Mwakitalu na Profesa Ngowi ambapo wawakilishi kutoka makampuni na mashirika mbalimbali walipata nafasi ya kuuliza maswali kutokana na mijadala hiyo.



*Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na watu wenye ulemavu Mheshimiwa Antony Mavunde akizungumza na mjasiriamali wakati wa maonyesho ya VICOBA katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es salaam.*

Kulikuwa na uwakilishi kutoka benki ya NMB, SIDO, PPF, CARE na wadau wengine wa maendeleo walishiriki kikamilifu katika zoezi zima la kuelimisha wana VICOBA na wananchi kwa ujumla.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji, Bi Beng'i Issa, alisema kuwa lengo la siku ya VICOBA ni kutambua, kuhamasisha na kuendeleza mifumo ya vikundi vya kuweka akiba na kukopesha kwa ajili ya kupata mitaji ya kufanya shughuli za kiuchumi ili kuchangia juhudi za kuondoa umasikini nchini.

"Tumeamua kufanya tukio hili ili kutambua mchango wa VICOBA kwa wananchi katika harakati za kujikwamua kiuchumi kama kauli mbiu yetu inavyosema 'VICOBA kwa maendeleo ya Taifa,'alisema Katibu Mtendaji.




*Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Charles Mwijage akitoa maelekezo kwa mjasiriamali katika siku ya maonyesho vya VICOBA yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es salaam.*

Tukio hilo litaendelea kuratibiwa na Baraza kila mwaka kwa kushirikiana na vyama mwamvuli vya kulea VICOBA ikiwa kama sehemu ya majukumu yake muhimu ya kutekeleza sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ya mwaka 2004.

# Baraza latoa mafunzo ya uanzishwaji wa madawati



Mafunzo ya viongozi na waratibu wa madawati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yakihusisha mikoa ya Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Iringa na Njombe yametolewa na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ili kufanikisha utekelezaji wa sera ya Uwezeshaji ya mwaka 2004.

Mafunzo hayo ya siku nne yalianza kufanyika tarehe 19-22 Septemba mwaka huu baada ya kuzinduliwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Amina Masenza katika ukumbi wa "Siasa ni Kilimo" uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa

Miongoni mwa watu muhimu waliohudhuria mafunzo hayo ni pamoja na Wakuu wa Mikoa 6, Makatibu Tawala 4, Wakuu wa Wilaya 21, Wakurugenzi wa Halmashauri 28, Maafisa Mipango 31, Waratibu wa uwezeshaji wa Mikoa na Halmashauri 35.

Katika kufungua mafunzo hayo, Katibu Mtendaji wa Baraza, Bibi Beng'i Issa aliwashukuru viongozi na watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa kwa maandalizi mazuri ya mafunzo na viongozi wote na waratibu wa uwezeshaji katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri kwa kukubali kuhudhuria mafunzo hayo.

Baraza la Uwezeshaji lililenga kuwajengea uwezo waratibu wa uwezeshaji ili kutafuta namna bora ya kuwa na mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004,kutoa muongozo wa uwezeshaji katika Halmashauri/ Manispaa/Miji/Majiji,Mifuko ya Uwezeshaji na Programu za Mitaji,kuongeza Ushiriki wa Watanzania katika Uwekezaji na Uanzishwaji Vikundi vya VICOBA.




*Baadhi ya washiriki wakifuatilia mafunzo ya madawati ya uwezeshaji yaliyofanyika nyanda za juu Kusini na kuratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi*

Katika mafunzo hayo, washiriki walipata nafasi ya kujadili mada baada ya uwasilishaji wa kila mada ili kuongeza uelewa kwa washiriki juu ya mada husika ambapo waliweza kuuliza maswali mbalimbali kwa wawezeshaji ili kupata ufafanuzi juu ya mada husika.

Wawezeshaji walitoa kazi kwenye vikundi na kutoa michango yao ili kuboresha fomu za ukusanyaji na uwasilishaji wa taarifa za uwezeshaji pamoja na Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini.

Wakati wa kuhitimisha mafunzo,ilifanyika tathmini ili kujua washiriki walielewa kwa kiasi gani mada zilizotolewa ambapo matokeo yake yalionyesha kuwa 98.5% ya washiriki wa mafunzo wameonesha kuwa yamewaongezea uelewa na stadi juu ya majukumu yao kama waratibu.

Aidha, 98.5% ya washiriki waliahidi kutumia stadi walizozipata katika mafunzo ili kuboresha utendaji wao wa kazi pamoja na kuboresha ushirikiano na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yao.

"Waratibu wa madawati ya Uwezeshaji watalisaidia Baraza katika kufuatilia na kuratibu shughuli za Uwezeshaji katika maeneo yao, hivyo mafunzo haya kwa viongozi ni muhimu ili waweze kuwasimamia vema waratibu wa madawati ya uwezeshaji"alisema Katibu Mtendaji.

"Ninawashukuru waratibu wa mafunzo na viongozi wote waliohudhuria mafunzo haya kwani Baraza lina wajibu wa kufanya kazi kwa kushirikiana na Mikoa na Halmashauri ili kuwafikia wananchi wote kwa urahisi" alisema Katibu Mtendaji.



# Profesa Kamuzora awahasa Watanzania kupiga vita umasikini

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu, Profesa Faustine Kamuzora amewataka Watanzania kuwa vinara katika kupiga vita umasikini kwa kutumia fursa za uwekezaji zilizopo nchini na kutoridhika na kipato kidogo.

Katibu Mkuu amesema hayo wakati alipotembelea ofisi za Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mara ya kwanza tangu alipoteuliwa kuchukua nafasi hiyo.



***Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu, Profesa Faustine Kamuzora***

"Tunazo fursa nyingi kama Taifa ambazo kila mmoja anaweza kutimiza ndoto zake za kiuchumi na kuwa tajiri. Moja ya fursa hizi ni uwepo wa rasilimali nyingi ambazo zinahitaji kuchakatwa na kuuza bidhaa zilizoongezwa thamani"alisema Katibu Mkuu.

Katibu Mkuu pia aliwaeleza watumishi wa Baraza kuendelea kufanyakazi kwa weledi ili kutimiza malengo ya Serikali katika kujenga uchumi bora na kuchochea maendeleo ya Taifa.

Aliwataka watumishi wa baraza hilo kuendelea kufanya kazi kwa weledi na kwa ushirikiano mkubwa ili kutimiza malengo ya Serikali katika kujenga uchumi bora na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Alisema fursa nyingine zilizopo ni pamoja na kuwepo kwa mifuko ya uwezeshaji 19, taasisi za kifedha yaani mabenki na soko kubwa la ndani na nje ya nchi ambalo kama litatumika vema linaweza kusogeza mbele gurudumu la maendeleo ya Kiuchumi.

Akifafanua zaidi, alisema Tanzania imejaliwa kuwa na kila aina ya rasilimali, hivyo wananchi wakizichangamkia suala la kuuza mali ghafi nje litafikia ukomo.

Mwishoni mwa Oktoba mwaka huu, Profesa Kamuzora aliteuliwa kushika wadhifa huo akitokea Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa wadhifa kama huo.




***Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Bibi Beng'i Issa akisaini hati ya makubaliano ya sheria za ununuzi wa Umma na Afisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Dk. Laurent Shirima***

# NEEC yaingia makubaliano na PPRA kuwainua wazabuni wa ndani

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limeingia makubaliano ya ushirikiano na Mamlaka ya ununuzi wa Umma (PPRA) kwa lengo la kuongeza ushiriki wa wafanyabiashara wadogo na wa kati katika ununuzi wa Umma.

Makubaliano hayo yamefikiwa ili kuwavuta wafanyabiashara wazawa katika ununuzi wa umma na kufungua milango kwa wazabuni wa ndani.

Wakati wa kusaini hati ya makubaliano hayo, Katibu mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Bi Beng'i Issa alisema kuwa lengo ni kutatua changamoto za wafanyabishara na kuwajengea uwezo waweze kufahamu namna ya kushiriki zabuni za Umma.

Bi Beng'i Issa alisema kuwa miongoni mwa fursa zitakazopatikana kwa wafanyabiashara wadogo na wakati katika Taasisi za Umma ni pamoja na huduma za usafi,chakula, ulinzi na uuzaji wa samani na vifaa vingine vya ofisi.

“Wafanyabiashara wengi hawaelewi fursa zilizopo kwenye mashirika ya umma na utaratibu wa kushiriki zabuni, wanashindwa kutimiza masharti kutokana na kukosa mitaji na maarifa hivyo makubaliano haya yataweza kufikia wafanyabiashara wa kada zote kushiriki zabuni kwenye Taasisi za umma pasipokuwa na pingamizi lolote”alisema Katibu Mtendaji

Afisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, DK Laurent Shirima amesema kuwa Taasisi hiyo itahakikisha michakato ya ununuzi inayofanywa na Taasisi za Umma inaendeshwa kwa misingi ya haki, ushindani na kuzingatia uwazi.

DK Shirima aliongeza kwamba kutakuwa na upendeleo kwa wazabuni wa ndani wakiwemo watu wanaotoka kwenye makundi maalumu ya walemavu, wanawake, wazee na kada ya vijana.

Katika makubaliano hayo ya Baraza na PPRA manunuzi yote yenye thamani ya chini ya Tshs 2 bilioni kipaumbele kitatolewa kwa wazabuni wa ndani.

Baraza linaendelea kuratibu sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kuhakikisha Watanzania wanapata nafasi ya kushiriki uchumi wa nchi kwa kuondolewa vikwazo mbalimbali.




*Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Bibi Beng’i Isaa akikabishiana hati ya makubaliano ya ununzi wa Umma na Afisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, DK Laurent Shirima.*

# Mkakati wa kuendeleza ujasiriamali wazinduliwa




SERIKALI kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limefanikiwa kuzindua mkakati jumuishi wa kuendeleza Ujasiriamali nchini ili kuchochea mapinduzi ya viwanda na uchumi wa kati.

Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Stela Manyanya alisema kuwa lengo la mkakati huo ni kusukuma mbele jitihada za Serikali katika kuwawezesha wananchi wake kiuchumi.

Alisema katika kufikia uchumi wa viwanda ni muhimu kwa wananchi kupitia ujasiriamali wao kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi ambayo ndio njia pekee na ya uhakika ya kuwawezesha wananchi wa kawaida kushiriki na kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wake.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni usimamizi wa biashara nchini,ujuzi,na elimu katika ujasiriamali, teknolojia na ubunifu, upatikanaji wa mitaji na ujengaji wa mitandao ya uhamasishaji.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Bibi Beng'i Issa alisema ili kuongeza ujuzi na maarifa ya ujasirimali kwa makundi mbalimbali Baraza limeandaa muongozo wa ufundishaji ambao pia utatumika kwenye sekta isiyo rasmi, elimu ya awali, msingi na vyuo vya elimu.

Nae Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Bwana Godfrey Sembeye alisema kuwa ni muhimu kuanza kufundisha ujasiriamali kwenye shule za msingi ili dhana ya ujasiriamali ianze kujengwa kwa vijana wa rika dogo.




***Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Stela Manyanya akiongoza zoezi la uzinduzi wa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ujasiriamali nchini.;'***

# HABARI KATIKA PICHA



*Wanachama wa VICOBA wakifuatilia maelekezo kutoka kwa Muwezeshaji katika siku ya Kilele ya VICOBA iliyofanyika katika*




*Maadhimisho ya Siku ya VICOBA katika Ukumbi wa Mliman City Jijini Dar es Salaam*



*Wajasiriamali kutoka katika vikundi vya VI-COBA wakinadi bidhaa zao katika viwanja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es salaam.*




*Naibu waziri  wa Nchi Ofisi ya waziri mkuu (kazi, Vijana na ajira) mheshimiwa Antony Mavunde akizungumza jambo na watumishi wa Benki ya wanawake TWB katika siku ya VICOBA*

# HABARI KATIKA PICHA




***Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Stela Manyara akigawa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ujasiriamali nchini***




***Washiriki wa tukio la uzinduzi wa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ujasiriamali nchini wakiwa katika picha ya pamoja***




***Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Stela Manyara aki-gawa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ujasiriamali nchini***




***Afisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, DK Laurent Shirima akizungumza jambo wakati wa ma-kubaliano ya sheria ya ununuzi wa Umma.Kushoto ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Bibi Beng'i Issa***

# HABARI KATIKA PICHA




***Profesa Honest Ngowi akitoa mada siku ya VICOBA Tanzania katika ukumbi wa Mliman City***



***Wanachama wa VICOBA wakikabidhi zawadi kwa Serikali kutokana na mchango wake kwa vikundi hivyo***




***Watoa mada wakifatilia mjadala katika ukumbi wa Mliman City jijini Dar es salaam katika uzinduzi wa siku ya VICOBA***



***Washiriki wa uzinduzi wa siku ya VICOBA katika ukumbi wa Mliman City***

## Baraza La Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

**S.L.P 1734**
**Mtaa wa kivukoni**
**Dar es Salaam-Tanzania**
**Simu/nukushi:+225 22 2125596**
**Barua Pepe: neec@uwezeshaji.go.tz**
**Tovuti: www.uwezeshaji.go.tz**
**Facebook:NEEC**
**Twiter:neec@empowerment**
**Youtube:Uwezeshaji**

**NEEC**

***NEEC Tanzania***

**Uwezeshaji**